

Kujua idadi ya Wanyama

Husaidia Uhifadhi Endelevu




Kuhusu CIMU

Conservation Information Monitoring Unit (CIMU) ni kitengo cha Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori kinachojishughukisha na kukusanya taarifa juu ya idjadi ya makazi ya wanyamapori ndani na kandokando ya maeneo yaliohifadhiwa nchini.



Madhumuni ya CIMU


- Kufanya tathmini ya idadi ya wanyamapori na maliasili nyingine zilizopo ndani au karibu na maeneo ya uhifadhi kutoka angani au ardhini
- Kutoa ushauri kutokana na matokeo ya utafiti
- Kufanya utafiti na kuboresha mbinu za kutadhimini idadi za wanyamapori
- Kukusanya, kuchanganua, kutunza na kuratibu kumbukumbu za wanyamapori



Huduma zitolewazo na CIMU

- Kuhesabu idadi ya wanyamapori kwa kutumia njia za angani na ardhini
- Kuendesha kozi fupi kuhusu GIS na matumizi ya ArcView na ArcGIS

Mbinu kuu za kuhesabu zitumiwazo na kitengo cha CIMU



Kuhesabu Eneo Lote

Njia hii hutumika kuhesabu wanyama waishio katika makundi makubwa kama tembo na mbogo. Picha hizi huunganishwa na kisha wanyama huhesabiwa mmoja mmoja katika picha zote.



Kuhesabu Sehemu ya Eneo

Sehemu ya eneo hukaguliwa na wanyama wote huhesabiwa. Idadi hiyo hutumika kukadiria hesabu ya wanyama waliopo katika eneo lote.



Kuhesabu Sehemu ya Kundu

Njia hii ni muafaka kwa wanyama wanaoishi katika makundi makubwa katika eneo kubwa kama vile nyumbu. Picha hupigwa kwa utaratibu na muda maalumu. Wanyama katika kila picha huhesabiwa na jumla yote hukadiriwa.

For more information, contact us through:
Box 661 Arusha
Tel: +255 27 254 9571
Email: info@tawiri.or.tz
Website: www.tawiri.or.tz